

# Inashangaza (Perplexing)

Mabango mengi na bidhaa zingine za mabango zimepigwa chapa na nembo yetu kwa kuonyesha, "Tunajivunia imetengenezwa Tanzania na Sign Industries" Nembo imewekwa kwa uangalifu kwenye uso wa mbele, kona ya mbali sana kwa upande na kufanya saizi ndogo ili isionekane kirahisi.

Wakati mabango yetu yanapowasilishwa na kupachikwa kwenye eneo la mteja, wakati mwingine kuna wateja fulani ambao hawakubali tuweke chapa yetu. Ni wazi tunaheshimu mapendekezo yao, na tunakubali kutokuweka.

Lakini kwa uaminifu wote, mawazo kama haya yanatumiza kwa nini wanachukia sisi kupachika nembo yetu, ambavyo vitu vingine vyote wanavyotumia kama iPhone vinaonyesha alama ndogo ya apple, Kompyuta zao zinaonyesha chapa kama Apple, DELL, HP, magari na vans zina alama zao mbele na nyuma pia. lifti za kwenye majengo, ngazi za mkanda huonyesha wazi chapa ya mtengenezaji na hata vitu vyatya madukani kama kalamu, saa ya mkono, mikoba, mashati na hata nguo zote hubeba nembo za wazalishaji na hazina pingamizi, lakini linapokuja suala la kuweka nembo yetu kwenye bidhaa tuliyotengeneza, wanapinga . Inasikitisha sana ni bora usitupongeze lakini uruhusu tuweke nembo yetu kwenye bidhaa tuliyotengeneza wenyewe hapa nchini na tujivunie kwa hilo.

Wakati mmoja nilipojadili shida hii na mteja, waliniambia kwamba wangependa kuonyesha kwamba bidhaa imeingizwa kutoka nje ya nchi, sio iliyotengenezwa nchini na watu wengi huamini kwamba kinachotoka nje ndio bora na hivyo huamini kwa urahisi. Lakini tena, bado inanichanganya kwanini sisi watanzania hata baada ya miaka 65 ya uhuru bado tujisikie fahari kwa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje na tusijivunie kwa bidhaa iliyotengenezwa hapa ambayo inakidhi kiwango cha kimataifa?

***Meneja wa eneo***